**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA KILIMO**

**TUME YA MAENDELEO YA USHIRIKA TANZANIA**

*Unapojibu, tafadhali taja:*
**Kumb. Na. LA. 93/288/01/109**

12 Novemba, 2024

Wenyeviti na Wajumbe wa Bodi,
Vyama vya Ushirika,
**TANZANIA BARA**

Yah: **WARAKA WA MRAJIS NA. 10 WA MWAKA 2024 KUHUSU KAMPUNI BINAFSI ZA UKAGUZI KURUHUSIWA KUFANYA UKAGUZI WA NJE KWENYE VYAMA VYA USHIRIKA**

**1.0 UTANGULIZI**

Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) imeweka utaratibu wa kushirikiana na wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na sekta binafsi, kuviwezesha Vyama vya Ushirika nchini kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi. Kutokana na utaratibu huo, Tume hutoa fursa kwa taasisi na kampuni mbalimbali zenye ueledi, uzoefu na ubobezi kwenye huduma wanazozitoa, kushirikiana nayo ili kuboresha na kuimarisha utendaji kazi katika Vyama vya Ushirika nchini.

Utaratibu huu upo kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya mwaka 2013 kifungu cha 4, kifungu cha 9(b) na kifungu cha 18. Vifungu hivi vya Sheria vinaipatia mamlaka Tume, kushirikiana wadau mbali mbali ili kuviwezesha Vyama vya Ushirika kutoa huduma bora zaidi zenye ufanisi na tija kwa Vyama, wanachama na jamii kwa ujumla.

Kwa mujibu wa kifungu cha 55(3) cha sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya Mwaka 2013, Vyama vya Ushirika, isipokuwa Benki ya Ushirika, vinapaswa kukaguliwa mara moja kwa mwaka na Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (COASCO) au taasisi nyingine ya ukaguzi iliyosajiliwa, ambayo imechaguliwa na Mkutano Mkuu wa Chama cha Ushirika na kuidhinishwa na Mrajis wa Vyama vya Ushirika nchini. Hata Hivyo inatarajiwa kwamba maamuzi ya Mkutano Mkuu wa wanachama yakiambatana na sababu za msingi zilizopelekea maamuzi ya kuchagua taasisi binafsi ya ukaguzi, yapelekwe kwa Mrajis wa

Vyama vya Ushirika ambaye baada ya kuyapitia na kuyatafakari atatoa kibali kwa taasisi hiyo kuruhusiwa kukagua Chama husika.

Aidha, itakumbukwa kuwa TCDC iliwahi kutoa waraka wa Mrajis Namba 1 wa mwaka 2015 ambao ulijulikana kama, ***Waraka wa Mrajis wa Vyama vya Ushirika Na 1 wa Mwaka 2015 kuhusu utaratibu wa Utoaji Vibali kwa Makampuni binafsi yanayojishughulisha na ukaguzi wa Vyama vya Ushirika.*** Waraka huu uliruhusu Vyama vya Ushirika kukaguliwa na Kampuni binafsi za Ukaguzi kwa utaratibu maalum uliokua umewekwa.

Utaratibu huu ulikoma kutumika baada ya kufutwa mnamo mwaka 2019 kufuatia maelekezo ya Mrajis wa Vyama vya Ushirika ambayo yalizuia Vyama vya Ushirika kukaguliwa na Kampuni Binafsi na badala yake kazi hiyo ilielekezwa ifanywe na COASCO pekee hadi pale Tume kwa kushirikiana na wadau, itakapokuwa imekamilisha kuandaa utaratibu mzuri utakaowawezesha Wakaguzi wa Nje kufanya vyema kazi ya ukaguzi katika Vyama vya Ushirika nchini.

## 2.0 DOSARI ZILIZOPO KATIKA MFUMO ULIOPO WA KUTOTUMIA WAKAGUZI BINAFSI

Kutokana na taarifa na takwimu za ukaguzi wa nje zilizopo, katika kipindi cha miaka mitatu ya hivi karibuni kuanzia mwaka 2020/2021 hadi 2022/2023, takwimu hizo zinaonesha kwamba idadi ya Vyama vya Ushirika vilivyofikiwa na kufanyiwa Ukaguzi wa Nje ni ndogo ikilinganishwa na idadi ya Vyama vilivyosajiliwa; kama inavyoonekana kwenye Jedwali hapa chini:-

**Jedwali: VYAMA VILIVYOFANYIWA UKAGUZI WA NJE 2020 - 2023**

| MWAKA WA FEDHA | VYAMA VILIVYOPO | VYAMA VILIVYO KAGULIWA | TOFAUTI |
|---|---|---|---|
| **2020/2021** | 9,315 | 6,013 | 3,302 |
| **2021/2022** | 9,525 | 6,005 | 3,520 |
| **2022/2023** | 7,349 | 3,878 | 3,471 |

Kutokana na hali hii ni wazi kwamba wakaguzi binafsi wanatakiwa kuruhusiwa kufanya kazi ili kuziba pengo lililopo la wastani wa Vyama 3,400 ambavyo havikaguliwi kwa kila mwaka. Aidha, ili kuongeza ushindani na ufanisi katika utoaji huduma ya ukaguzi unaofanyika, ubunifu, ukuaji wa sekta pamoja na kuendana na mabadiliko yanayoendelea kutokea kwenye sekta, Ofisi ya Mrajis imeona ni vyema taasisi binafsi za ukaguzi zikaruhusiwa kufanya kazi hiyo kwenye Vyama vya Ushirika kwa mujibu wa Sheria, kanuni na miongozo ya Ushirika ili kuongeza ufanisi na kuendelea kujenga imani kwa umma kuhusu mwelekeo na maendeleo ya Ushirika nchini.

**3.0 MALENGO YA WARAKA**

Lengo kuu la waraka huu ni kufuta Waraka wa awali wa Mrajis uliotolewa kuzuia Kampuni binafsi za Ukaguzi kufanya Ukaguzi wa Nje kwenye Vyama vya Ushirika. Aidha, waraka huu unaruhusu huduma ya ukaguzi wa nje kuongezwa katika orodha ya huduma zinazotolewa na watoa huduma kwenye Vyama vya Ushirika nchini. Kwa muktadha huo, Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania imeandaa utaratibu wa kuwapata wakaguzi binafsi watakaotoa huduma za ukaguzi kwenye Vyama vya Ushirika kwa kuzingatia malengo yafuatayo:

i. Kuweka Udhibiti katika utoaji wa Vibali kwa wakaguzi wa nje wa Vyama vya Ushirika
ii. Kuweka Utaratibu maalum wa kupokea, kuhakiki na kutolea maamuzi maombi ya vibali vya kufanya ukaguzi wa nje kwenye Vyama vya Ushirika.
iii. Kuhakikisha unakuwepo ubora wa huduma za ukaguzi wa nje zinazotolewa kwa Vyama vya Ushirika na wakaguzi binafsi.
iv. Kuwa na utaratibu mzuri wa kufanya tathmini ya kina ya utendaji kazi wa taasisi binafsi zitakazopewa vibali vya kufanya ukaguzi wa nje na Mrajis wa Vyama vya Ushirika nchini kila mwaka.
v. Kuorodhesha Kampuni/Taasisi zote zitakazopewa vibali vya kufanya ukaguzi wa nje kwenye Vyama vya Ushirika na kuzitangaza kwa umma kwa lengo la kudhibiti na kuweka wazi taarifa zake.

## 4.0 UTARATIBU UTAKAOTUMIKA KATIKA UTOAJI WA VIBALI KWA WAKAGUZI WA NJE

Utaratibu utakaotumika kuwapata Watoa Huduma ya Ushauri na Ukaguzi wa Hesabu utakuwa ni wa kawaida ambao unatumika katika kuwapata watoa huduma wengine. Hatua hizo ni kama zifuatazo:

1. Mtoa huduma kutuma maombi (Kupitia mfumo wa MUVU) ya kutoa huduma katika eneo la Ushauri na Ukaguzi wa Hesabu ambapo, pamoja na barua ya maombi, mhusika atapaswa kuambatisha vielelezo muhimu vinavyothibitisha uhalali wa uwepo wa kampuni yake kisheria (Hati ya Usajili, Namba ya Utambulisho wa Mlipa kodi, Cheti cha Mlipa kodi, Leseni ya biashara, Wasifu wa Wakurugenzi na Watendaji wa Kampuni na Hati ya Ithibati ya Kitaaluma ya NBAA). Aidha atawasilisha maelezo ya Kampuni (Company Profile) pamoja na taarifa nyingine kama itakavyoainishwa kwenye Mwongozo wa Watoa Huduma ya Ushauri na Ukaguzi wa Hesabu kwenye Vyama vya Ushirika.
2. Hatua ya pili itakuwa ni usaili ambapo jopo la usaili litaundwa na Mrajis wa Vyama vya Ushirika kwa kuzingatia Mwongozo wa watoa Huduma ya ushauri na ukaguzi wa Hesabu kwenye Vyama vya Ushirika.
3. TCDC itaweka masharti ya kiwango cha chini (Minimum Qualifications) ya sifa na vigezo vinavyopaswa kufikiwa kabla Kampuni haijapewa kazi ya kutoa huduma ya ushauri na ukaguzi kwenye Vyama vya Ushirika.

4. Vibali vitakavyotolewa na Mrajis wa Vyama vya Ushirika, vitakua na masharti maalum kwa watoa huduma ya ushauri na ukaguzi kwenye Vyama vya Ushirika na watapaswa kuwajibishwa kwa ukiukaji wa masharti hayo pale itakapo bainika wamekiuka sehemu ya masharti hayo.

5. COASCO itaendelea kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria yake ikiwemo kuishauri Tume mara kwa mara kuhusu mwenendo wa utekelezaji wa kazi za wakaguzi binafsi wa nje ambao watakuwa wamepewa vibali vya ukaguzi na Mrajis wa Vyama vya Ushirika nchini.

6. Warajis Wasaidizi wa Mikoa watatumiwa nakala za barua za kutoa vibali kwa watoa huduma kwa ajili ya rejea, usimamizi na ufuatiliaji wa karibu.

## 5.0 UTEKELEZAJI WA WARAKA

Waraka huu utatekelezwa na Vyama vyote vya Ushirika chini ya Usimamizi wa Warajis Wasaidizi wa Mikoa na Maafisa Ushirika.

## 6.0 MUDA WA UTEKELEZAJI

Waraka huu utaanza kutekelezwa, mara tu baada ya kusainiwa na Mrajis wa Vyama vya Ushirika. Aidha, kila mwaka itafanyika tathmini ya utekelezaji wake.

## 7.0 HITIMISHO

Ikumbukwe kwamba ni jukumu la Warajis Wasaidizi kuhakikisha kuwa Vyama vya Ushirika vyote nchini vinakaguliwa kila mwaka na Mkaguzi wa Nje ambaye atakuwa ni COASCO au Kampuni/Taasisi binafsi ya ukaguzi itakayokuwa imepewa kibali na Mrajis wa Vyama vya Ushirika nchini. Aidha, Warajis Wasaidizi wa mikoa wanapaswa kuhakikisha kuwa taarifa za ukaguzi uliofanyika, zinasomwa katika mikutano mikuu ya Vyama vya Ushirika kwa kuzingatia Sheria ya Vyama vya Ushirika. Kwa hali hiyo, Warajis Wasaidizi wanakumbushwa kutoa taarifa za hali ya kaguzi za Vyama vya Ushirika katika mikoa yao kila mwaka, kabla ya mwezi Aprili ili zijumuishwe katika taarifa ya jumla ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika.

8. Nawatakiea utekelezaji mwema.

Dkt. Benson Ndiege
**MRAJIS WA VYAMA VYA USHIRIKA**

**Nakala:** Mhe. Hussein Bashe (Mb),
Waziri wa Kilimo,
Mji wa Serikali - Mtumba,
S.L.P 2182,
**DODOMA**

Katibu Mkuu,
Wizara ya Kilimo,
Mji wa Serikali - Mtumba,
S.L.P 2182,
**DODOMA**

Naibu Katibu Mkuu (Ushirika na Umwagiliaji),
Wizara ya Kilimo,
Mji wa Serikali - Mtumba,
S.L.P 2182,
**DODOMA**

Abdul Majid Nsekela,
Mwenyekiti wa Kamisheni,
Tume ya Maendeleo ya Ushirika,
S.L.P 201,
**DODOMA**

Mkurugenzi Mkuu,
Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika,
S.L.P 761,
**DODOMA**

Warajis Wasaidizi wa Vyama vya Ushirika Mikoa,
**TANZANIA BARA**

Maafisa Ushirika wote,
**TANZANIA BARA** *(Kwa ufuatiliaji na Usimamizi)*

Mwenyekiti na Wajumbe wa Bodi,
Shirikisho la Vyama vya Ushirika Tanzania,
S.L.P 2567,
**DAR ES SALAAM**

Mwenyekiti na Wajumbe wa Bodi,
Muungano wa Vyama vya Ushirika wa
Akiba na Mikopo (SCCULT),
S.L.P 20640,
**DAR ES SALAAM**